TANGAZO LA SERIKALI Na. 787 la tarehe.

SHERIA YA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA,

(SURA YA 272)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 9(1) na (2))*

NOTISI YA KUONGEZA ENEO LA HUDUMA LA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BUSEGA YA MWAKA 2024

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kuongeza Eneo la Huduma la Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Busega ya Mwaka 2024.

Kuongeza eneo la huduma

2. Eneo la Huduma la Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Busega linaongezwa kujumuisha eneo lililoainishwa katika Jedwali l.

Kukoma kwa huduma

3.-(1) Chombo chochote ngazi ya jamii au chombo kilichosajiliwa kabla ya kuanza kutumika kwa Notisi hii kutoa Huduma za maji safi na usafi wa mazingira katika eneo lililoainishwa katika Jedwali, kitaacha kutoa Huduma.

(2) Haki, majukumu, masharti ya ajira ya watumishi, mali, madeni na masuala yanayohusika yaliyopokelewa, kutolewa au yanayotekelezwa na chombo ngazi ya jamii au chombo kilichotajwa chini ya aya ya 3 (1) vitabaki chini ya himaya ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Busega.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(1))*

| JINA LA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA | ENEO LINALOONGEZWA | |
|---|---|---|
| | WILAYA YA BUSEGA MKOA WA BARIADI | |
| MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA BUSEGA | KATA | KIJIJI |
| | 1. Kaloleli | 1. Ijitu<br>2. Ihale<br>3. Yitwimila 'A'<br>4. Ilumya<br>5. Yitwimila 'B' |
| | 2. Mwamanyili | 1. Milambi<br>2. Nassa Ginnery<br>3. Mwanangi<br>4. Mwamanyili |
| | 3. Kabita | 1. Nyakaboja<br>2. Kabita<br>3. Nyamikoma<br>4. Shimanilwe |
| | 4. Lutubiga | 1. Mwasamba<br>2. Mwangika<br>3. Lutubiga<br>4. Mwakiloba |

Dodoma,
13 Agosti, 2024

JUMAA H. AWESO,
*Waziri wa Maji*